

# Zab117 - HII NDIO SIKU ALIYOIFANYA BWANA

Siku kuu ya Paska

Eugène AMPIRE




1. Mshukuruni Bwana kwani ndiye mwema,
   Kwani wema wake ndio wa milele.
   Wenye kumwabudu Bwana waseme:
   Kweli wema wake ndio wa milele.

2. Mkono wa kuume wa Bwana umetukuzwa,
   Mkono wa kuume wa Bwana umetenda makubwa.
   Sitakufa, lakini nitaishi,
   Tena nitahubiri matendo ya Bwana.

3. Jiwe walilokataa wajengaji,
   Hilo limekuwa jiwe la pembe :
   Ndilo jambo alilofanya Bwana,
   Nasi twaliona ajabu.